
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KOROSHO TANZANIA




# JARIDA LA KOROSHO MWEZI MEI 2023



TOLEO NA. CBT 009

IMEANDALIWA NA BODI YA KOROSHO TANZANIA

## 1.0 UTANGULIZI

Msimu wa Mauzo ya Korosho nchini Tanzania unakaribia kufikia tamati baada ya mauzo katika mikoa ya Tanga, Dodoma na Singida ambayo Msimu huanza mwezi Februari kufikia mwisho mwezi Mei.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi sasa zaidi ya tani 169,071.832 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 155,963,669.88 (FOB Value) zimeombewa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 2,017.586 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 52,383,549.57 (FOB Value) zimesafirishwa.


## 2.0. MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast, kiasi kikubwa cha korosho kimeuzwa na hakuna mahitaji makubwa kutoka kwa wanunuzi wa nje. Kwa mwezi Mei bei ya korosho ghafi kwa mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.25 hadi 0.41 kwa kilogramu kulingana na eneo. Katika kipindi cha mwezi Machi hadi Aprili Ivory Coast imesafirisha takribani tani 335,000 za korosho ghafi, huku Vietnam ikiongoza kwa kununua kiasi kingi kutoka Ivory Coast ambapo imenunua jumla ya tani 237,727 ikifuatiwa na India iliyonunua tani 97,242.

**Jedwali Na. 1: Usafirishaji wa Korosho Ghafi Ivory Coast Kwenda India na Vietnam Kwa Kipindi cha Mwezi April, 2023**

| USAFIRISHAJI WA KOROSHO GHAFI IVORY COAST KWENDA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **NA.** | **NCHI** | **KIASI (TANI)** | **THAMANI (USD)** |
| 1 | India | 47,952.00 | 50,887,055.00 |
| 2 | Vietnam | 135,117.00 | 148,555,503.00 |
| | **Jumla Kuu** | **183,069.00** | **199,442,558.00** |




**Chanzo:** Cashewnutinformation

Nchini Ghana kampuni nyingi zimesimamisha ununuzi wa korosho ghafi, sababu kubwa ni kushuka kwa thamani ya *Cedis* dhidi ya Dola. Katika miezi miwili iliyopita (Machi-Aprili 2023), India imeagiza zaidi ya tani 74,000 za korosho ghafi kutoka Ghana.

Nchini Benin idhini ya kusafirisha korosho nje bado haijatolewa. Kampuni za ndani zinaendelea kununua korosho kwa ajili ya kuuza nje kwa tahadhari ya hali ya juu sana

kwa kuhofia uamuzi huo kutotenguliwa. Bei ya korosho kwa mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.37 hadi 0.56 kulingana na eneo na ubora wa korosho.

Nchini Burkina Faso mauzo ya korosho yameanza kushuka na bei ya korosho kwa mkulima kwa mwezi Mei imeshuka kidogo kutoka Dola za Kimarekani 0.47 hadi 0.50 kwa kilogramu kwa mwezi Aprili na kuwa Dola za Kimarekani 0.45 hadi 0. 49 kwa kilogramu.

## 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India


Bei za korosho ghafi imebaki kuwa thabiti na katika maeneo mbalimbali bei ni kati ya Dola za Kimarekani 0.98 hadi 1.21 kwa kilogramu kulingana na ubora na kiwango cha unyevu. Mahitaji ya ndani ya korosho karanga yanatarajiwa kuongezeka kuanzia katikati ya mwezi Juni na kuendelea.

## 2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam

Nchini Vietnam soko la korosho ghafi linaendelea kuwa la chini, hakuna manunuzi makubwa yanayoonekana kufanyika kwa siku za hivi karibuni na kuna baadhi ya ofa zinatolewa zikiwa na kiwango cha chini cha "SHOT" hivyo wanunuzi wengi hawaonyeshi kuvutiwa. Korosho ghafi yenye "SHOT" ya juu nayo imeshuka na kuuzwa hadi Dola za Kimarekani 1,100 kwa tani, madaraja yenye "SHOT" chini ya 46 yameuzwa chini ya Dola za Kimarekani 1,000 kwa tani.

**Jedwali Na. 2: Usafirishwaji wa Korosho Karanga Vietnam Kwenda Nchi Mbalimbali Kuanzia Januari hadi April, 2023**

| USAFIRISHWAJI WA KOROSHO KARANGA VIETNAM KWENDA NCHI MBALIMBALI KUANZIA JANUARI HADI APRILI- 2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI(TANI) | THAMANI (USD) | WASTANI USD/TANI |
| 1 | Marekani | 42,890.00 | 250,394,155.00 | 5,838 |
| 2 | China | 18,891.00 | 124,594,337.00 | 6,595 |
| 3 | Uholanzi | 14,607.00 | 88,264,218.00 | 6,043 |
| 4 | Saudi Arabia | 4,941.00 | 29,422,367.00 | 5,955 |
| 5 | Uingereza | 5,557.00 | 28,901,698.00 | 5,201 |
| 6 | Ujerumani | 4,712.00 | 27,024,450.00 | 5,735 |
| 7 | Umoja wa Falme za Kiarabu | 5,618.00 | 32,428,248.00 | 5,772 |
| 8 | Australia | 3,835.00 | 20,883,900.00 | 5,446 |
| 9 | Canada | 3,885.00 | 23,624,554.00 | 6,081 |
| 10 | Iraq | 2,707.00 | 12,200,254.00 | 4,507 |
| 11 | Uhispania | 2,788.00 | 16,109,738.00 | 5,778 |
| 12 | Japani | 2,979.00 | 19,193,166.00 | 6,443 |
| 13 | Israeli | 2,184.00 | 14,575,997.00 | 6,674 |
| 14 | Thailand | 2,900.00 | 16,463,537.00 | 5,677 |
| 15 | Itali | 2,311.00 | 9,612,934.00 | 4,160 |
| 16 | Ufaransa | 2,287.00 | 14,628,195.00 | 6,396 |
| 17 | Taiwani | 1,692.00 | 11,386,393.00 | 6,730 |
| 18 | Urusi | 2,124.00 | 11,237,479.00 | 5,291 |
| 19 | India | 938.00 | 4,724,051.00 | 5,036 |
| 20 | Ugiriki | 1,164.00 | 6,680,456.00 | 5,739 |
| 21 | Ufilipino | 1,009.00 | 5,164,666.00 | 5,119 |
| 22 | Ubelgiji | 994.00 | 6,415,510.00 | 6,454 |
| 23 | Newzealand | 975.00 | 5,039,124.00 | 5,168 |
| 24 | Misri | 551.00 | 3,837,086.00 | 6,964 |
| 25 | Singapore | 361.00 | 2,205,062.00 | 6,108 |
| 26 | HongKong | 570.00 | 4,400,715.00 | 7,721 |
| 27 | Norway | 454.00 | 2,665,952.00 | 5,872 |
| 28 | Afrika Kusini | 230.00 | 1,289,331.00 | 5,606 |
| 29 | Kuwait | 226.00 | 1,525,324.00 | 6,749 |
| 30 | Pakistan | 321.00 | 1,972,390.00 | 6,145 |
| 31 | Nchi Nyingine | 27,948.00 | 157,192,083.00 | 5,624 |
| | **Jumla kuu** | **162,649.00** | **954,057,370.00** | **5,891** |





**Chanzo:** Cashewnutinformation



**Jedwali Na.3: Bei za Korosho Ghafi katika Nchi ya India na Vietnam Mei, 2023**

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI (INDIA NA VIETNAM) KWA KIPINDI CHA NOVEMBA 2022 HADI MEI, 2023 | | |
|---|---|---|
| TAREHE | BEI-CIF USD/TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 05 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 27 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 12 Desemba, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| 24 Desemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 14 Januari, 2023 | 1,200 | 1,275 |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,390 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 Aprili, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| 20 Mei, 2023 | 1,040 | 1,130 |
| SOT: 46-52 | | |




**Chanzo:** Cashewnutinformation

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNIANINCHI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia Mei, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko madogo ya bei kwa mwezi Mei kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 4: Bei za Korosho Karanga Nchini Vietnam hadi kufikia Mei, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA MEI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | WW180 | 7.72 | 8.27 | 17,987.60 | 19,269.10 |
| White Whole Cashews 210 | WW210 | 6.84 | 7.28 | 15,937.20 | 16,962.40 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.84 | 6.28 | 13,607.20 | 14,632.40 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.47 | 5.84 | 12,745.10 | 13,607.20 |
| Large Pieces | LP | 3.31 | 3.64 | 7,712.30 | 8,481.20 |
| Small Pieces | SP | 2.43 | 2.87 | 5,661.90 | 6,687.10 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Mei, 2023

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni pamoja na Ivory Coast, Ghana na Benin ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 5: Bei ya Korosho Karanga Afrika Magharibi hadi Kufikia Mei, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA MEI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 210 | W210 | 7.72 | 7.94 | 17,987.60 | 18,500.20 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.84 | 6.06 | 13,607.20 | 14,119.80 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.62 | 5.73 | 13,094.60 | 13,350.90 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.18 | 5.40 | 12,069.40 | 12,582.00 |
| White Splits | WS | 4.19 | 4.63 | 9,762.70 | 10,787.90 |
| Large Pieces | LP | 2.98 | 3.20 | 6,943.40 | 7,456.00 |
| Small Pieces | SP | 2.54 | 2.87 | 5,918.20 | 6,687.10 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.3 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Mei, 2023

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni, Marekani nk. Ni kama ilivyo katika jedwali Na. 7


**Jedwali Na. 6: Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi hadi kufikia Aprili, 2023.**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA MEI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | 8.00 | 8.50 | 18,640.00 | 19,805.00 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 7.30 | 7.50 | 17,009.00 | 17,475.00 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 6.80 | 7.00 | 15,844.00 | 16,310.00 |
| White Splits | WS | 3.93 | 4.54 | 9,156.90 | 10,578.20 |
| Large White Pieces | LWP | 3.93 | 4.54 | 9,156.90 | 10,578.20 |

**Chanzo:** TACP

**Jedwali Namba 7: Uwiano Wa Bei Daraja WW320**

| UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nchi | Bei ya Chini Dola/Kilo | Bei ya Juu Dola/Kilo | Bei ya Chini Tzs/Kilo | Bei ya Juu Tzs/Kilo |
| Vietnam | 5.47 | 5.84 | 12,745.10 | 13,607.20 |
| Afrika Magharibi | 5.62 | 5.73 | 13,094.60 | 13,350.90 |
| Tanzania | 6.80 | 7.00 | 15,844.00 | 16,310.00 |




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2022/2023 ni tani 188,284.748 zenye thamani ya shilingi 346,513,124,490 ambapo tani 176,710.097 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 328,306,121,285. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi Mei ni tani 4,586.286 zenye thamani ya shilingi 7,724,456,650 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni takribani tani 1,552.969 sawa na tani 6,988.364 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 10,482,546,555. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.


**Jedwali Na. 8a: Taarifa ya Uzalishaji Korosho Msimu wa 2022/2023 Hadi Kufikia Mwezi Mei, 2023**

| TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA TAREHE 30/05/2023 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SN | MKOA | CHAMA KIKUU | GHALA ZA MNADA (KG) | THAMANI GHALA ZA MNADA (TSHS) | SOKO LA AWALI (KG) | THAMANI SOKO LA AWALI (TSHS) | ZILIZOBANGULIWA (KG) | | THAMANI UWIANO WA GHAFI (TSHS) |
| | | | | | | | ZILIZOBANGULIWA | UWIANO WA GHAFI | |
| 1 | MTWARA | TANECU | 33,518,494.00 | 63,447,865,104.00 | 1,486,294.00 | 2,411,476,400.00 | 962,460.50 | 4,331,072.25 | 6,496,608,375.00 |
| | | MAMCU | 59,609,667.00 | 111,449,764,229.00 | 931,022.00 | 1,571,913,400.00 | 116,881.00 | 525,964.50 | 788,946,750.00 |
| 2 | LINDI | RUNALI | 42,440,859.00 | 81,187,464,564.00 | 7,200.00 | 11,520,000.00 | 2,611.00 | 11,749.50 | 17,624,250.00 |
| | | LINDI MWAMBAO | 14,622,801.00 | 25,590,331,828.00 | 588,532.00 | 1,019,772,900.00 | 195,453.56 | 879,541.02 | 1,319,311,530.00 |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 15,156,209.00 | 26,809,585,960.00 | 126,446.00 | 191,965,000.00 | | - | - |
| 4 | PWANI | CORECU | 10,759,505.00 | 18,796,294,846.00 | 1,415,619.00 | 2,468,173,500.00 | 269,043.00 | 1,210,693.50 | 1,816,040,250.00 |
| 5 | TANGA | TACACU | 339,519.00 | 569,336,325.00 | | | 6,520.80 | 29,343.60 | 44,015,400.00 |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | 23,208.00 | 41,890,440.00 | 18,769.00 | 30,968,850.00 | | - | - |
| 7 | MOROGORO | MOFACU | 153,959.00 | 264,846,120.00 | | | | - | - |
| 8 | TABORA | | | | 2,000.00 | 3,000,000.00 | | - | - |
| 9 | DODOMA | DOMASIKA | 24,079.00 | 40,164,540.00 | | | | - | - |
| 10 | MBEYA | TAMCU | 25,850.00 | 45,418,450.00 | 404.00 | 666,600.00 | | - | - |
| 11 | NJOMBE | TAMCU | 35,947.00 | 63,158,879.00 | | | | - | |
| 12 | KIGOMA | | | | 10,000.00 | 15,000,000.00 | | - | - |
| | JUMLA NDOGO | | 176,710,097.00 | 328,306,121,285.00 | 4,586,286.00 | 7,724,456,650.00 | 1,552,969.86 | 6,988,364.37 | 10,482,546,555.00 |
| | JUMLA KUU UZALISHAJI | | | | | | | | 188,284,747.37 |
| | JUMLA KUU THAMANI | | | | | | | | 346,513,124,490.00 |

*NB: Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023. Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea.*

**Jedwali Na. 8b: Usafirishwaji wa Korosho Ghafi Tanzania Kwenda Nchi Mbalimbali Kuanzia Novemba 2022 hadi Mei, 2023**

| USAFIRISHWAJI WA KOROSHO GHAFI KUTOKA TANZANIA KWENDA NCHI MBALIMBALI KUANZIA NOVEMBA 2022 HADI MEI 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| NA. | NCHI | KIASI (KG) | THAMANI (USD FOB) |
| 1 | Vietnam | 95,052,933.00 | 87,097,874.40 |
| 2 | India | 73,654,114.00 | 68,629,495.48 |
| 3 | China | 314,160.00 | 184,800.00 |
| 4 | Bangladesh | 50,625.00 | 51,500.00 |
| | JUMLA | 169,071,832.00 | 155,963,669.88 |




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

**Jedwali Na. 8c: Korosho Zilizouzwa Kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.**

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani hadi Mei, 2023) | | |
|---|---|---|
| KIPINDI CHA | KIASI KILICHOUZWA (KG) | THAMANI (TZS) |
| Mwezi Mei | 23,208 | 41,890,440 |
| Jumlishi Oktoba-Aprili | 176,662,810 | 328,224,066,305 |
| Jumla | 176,686,018 | 328,265,956,745 |

**Jedwali Na. 8d: Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Minada**

| Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Mnada | | | |
|---|---|---|---|
| Mwezi Uliopita (Aprili, 2023) | | Mwezi wa Sasa (Mei, 2023) | |
| | Mwezi | Daraja la Kawaida | |
| | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| Mwenendo wa Bei | *Bei ya Mwezi Mei* | 1,805 | 1,805 |
| | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,720 | 1,720 |
| | *Mabadiliko (%)* | ▲4.9% | ▲4.9% |

## Jedwali Na. 8e: Bei za Mauzo ya Korosho Ghafi Kimkoa.

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Mei, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | MWEZI | Daraja la Kawaida | |
| | | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| MTWARA | MAMCU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,705 | 1,680 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| | TANECU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,605 | 1,604 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| LINDI | RUNALI | *Bei ya Mwezi Meii* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,770 | 1,600 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| | LINDI MWAMBAO | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,726 | 1,726 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| PWANI | CORECU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,520 | 1,520 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| RUVUMA | TAMCU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,605 | 1,605 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| MOROGORO | MOFACU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,721 | 1,721 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| TANGA | TACACU | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,719 | 1,719 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| DODOMA | DOMASIKA | *Bei ya Mwezi Mei* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | 1,720 | 1,720 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| SINGIDA | CEAMCU | *Bei ya Mwezi Mei* | 1,805 | 1,805 |
| | | *Bei ya Mwezi Aprili* | NA | NA |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |

**Ufunguo: NA = HAIPO**

Alama (▲▼►) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei. (▲) Bei imeongezeka; (▼) Bei imeshuka; (►) Hakuna mabadiliko ya bei.

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania
**2023**

## 5.0 UZINDUZI WA MBIO ZA KOROSHO (KOROSHO MARATHON) MSIMU WA PILI, 2023

Bodi ya Korosho inaendelea na maandalizi ya mbio za korosho (Korosho Marathon) kwa msimu wa pili. Uzinduzi wa mbio hizo umefanyika tarehe 13 Mei, 2023 katika Hoteli ya Luwa Evergreen na viwanja vya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kwa kugawa mashine mia moja (100) za kubangua korosho kwa vikundi vidogo vya ubanguaji wa korosho vya mkoa wa Mtwara na Lindi. Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika tarehe 2 Septemba, 2023 Mtwara mjini na malengo ya mbio hizo ni kuhamasisha ulaji wa korosho karanga na matumizi ya bidhaa zinazotokana na korosho nchini.



**Picha 01:** *Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed akigawa mashine za kubangua korosho kwa mwakilishi wa kikundi cha ubanguaji.*

## 6.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023

Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji korosho duniani, huku ikishika nafasi ya pili katika bara la Afrika na nafasi ya sita duniani kwa mujibu wa taarifa za African Cashew Alliance (2021). Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na maandalizi ya mkutano wa kimataifa wa korosho nchini utakaoitwa “Tanzania International Cashew Conference” utakaofanyika kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2023 hadi 14 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere.

Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha maendeleo ya zao la korosho kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika zao la korosho. Kupitia mkutano huo, inatarajiwa ushiriki wa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi katika Nyanja za utafiti, utengenezaji mashine za usindikaji, viwanda vya ubanguaji na uwekezaji. Mkutano huo utaenda sambamba na maonyesho ya bidhaa zitokanazo na zao la korosho na teknolojia mbalimbali zitumikazo katika usindikaji wa bidhaa za korosho.

## 7.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei tayari manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya wilaya Nanyamba na Halmashauri ya wilaya Tandahimba zimehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea na mpaka sasa jumla ya wakulima 111,192 wamefikiwa na kuhuishwa taarifa zao katika halmashauri nne kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho Kufikia Tarehe 31/05/2023.**

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Mtwara | 1,937.00 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Mtwara | 15,790.00 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya Nanyamba | 26,593.00 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya Tandahimba | 66,872.00 |
| | **Jumla** | **111,192.00** |

## 8.0 TAARIFA YA MAPOKEZI NA UGAWAJI PEMBEJEO ZA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2023/2024

Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na upokeaji na ugawaji wa pembejeo za zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2023/2024. Hadi kufikia tarehe 31 Mei tayari jumla ya lita 1,392,849 za viuatilifu vya maji, Sulphur ya unga tani 10,190 mabomba 5,000 na magunia 396,900 tayari vimeshapokelewa katika ghala za kupokelea pembejeo kitaifa zilizopo katika mikoa ya Mtwara na Lindi na Pwani. Ugawaji wa pembejeo umeanza kwa baadhi ya kata za Halmashauri ya wilaya ya Tandahimba, Newala, Masasi na halmashauri ya mji Nanyamba katika mkoa wa Mtwara pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Mtama katika mkoa wa Lindi.



***Picha Na.02***: Wakulima wa kijiji cha Namtumbuka Halmashauri ya Mji wa Nanyamba wakipokea Pembejeo za ruzuku zinazotolewa na serikali kwa ajili ya uzalishaji wa Korosho msimu wa 2023/2023




***Picha Na.03***: Salfa ikipakuliwa kwenye Meli yenye zaidi ya tani 3,680 katika bandari ya Mtwara kwa ajili ya uzalishaji wa Korosho msimu wa 2023/2024


MAWASILIANO:
MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA
Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450
Barua pepe: info@cashew.go.tz
Tovuti: www.cashew.go.tz